

DKT. MARY MWANJELWA ATEMBELEA OFISI ZA TAKUKURU

Naibu Waziri – Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora, Mhe Dkt. Mary Mwanjelwa ametembelea ofisi za TAKUKURU Dar es Salaam tarehe 8/01/2019.

Ziara hii ambayo imefanyika kwa siku moja imelenga katika kujitambulisha pamoja na kuyafahamu majukumu ya Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa ambayo ni moja ya Taasisi zilizoko chini ya Wizara anaoisimamia.



PICANI: Naibu Waziri Ofisi ya Rais Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora - Mhe. Dkt Mary Mwanjelwa akiwa katika picha ya pamoja na Viongozi wa TAKUKURU.

Pamoja na kutembelea Kurugenzi na ofisi mbalimbali za Taasisi, Naibu Waziri huyu alikutana na kuzungumza na watumishi wa TAKUKURU. Katika mazungumzo hayo, Dkt Mwanjelwa aliwasihi watumishi wa TAKUKURU kufanya kazi kwa uadilifu, weledi na uaminifu ili kumuunga mkono Mhe. Rais Dkt. John Pombe Magufuli katika mapambano dhidi ya rushwa nchini.

Vile vile Dkt. Mwanjelwa amewataka watumishi wa TAKUKURU kutenda haki katika chunguzi wanazozifanya kwani jamii inawategemea sana na wakati mwingine inawachukulia kama wakombozi wa wanyonge.

Mwisho, Naibu Waziri huyo ameipongeza taasisi hiyo kwa kazi nzuri inayoifanya ambayo inaunga mkono azma ya Mhe. Dkt John Pombe Magufuli Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya kuleta maendeleo kwa Watanzania.